

»Ufugaji wa njiwa kwa uwekezaji mdogo na kipato cha juu«

Kwa kuwa ni biashara yenye thamani na faida kubwa, wingi na ubora wa uzalishaji wa njiwa huamuliwa sana na mbinu ya usimamizi inayotumika.

Ufugajo wa njiwa huvutia, una faida na njiwa ni ndege maarufu. Hata hivyo tofauti na uwekezaji mwengine, ufugaji wa njiwa unahitaji vibarua kidogo na uwekezaji mdogo, na nyama ya njiwa ya ina ladha, lishe na wateja wengi.

Usimamizi wa njiwa

Kwa vile ufugaji wa njiwa ni chanzo kikubwa cha kipato cha ziada na burudani, njiwa wanaweza kuhifadhiwa kwenye nyumbani paa la nyumba. Huanza kutaga mayai baada ya miezi 6 na huangua watoto wawili kila mwezi kwa wastani. Kwa usimamizi bora, hakikisha kuna uingizaji mzuri wa hewa na mwanga ndani ya banda la njiwa.

Vile vile, banda linaweza kujengwa kwa vifaa vyatia kienyeji vinavyopatikana kwa urahisi. Kila njiwa huhitaji nafasi ya urefu wa 30cm, upana wa 30cm na kina hicho. Linda banda dhidi ya wanyama wawindaji, na kisha kuzuia maji kuingia moja kwa moja ndani banda.

Safisha banda mara moja au mbili kwa mwezi kwa afya bora ya njiwa. Ili kulisha njiwa, chakula kinapaswa kuwa na protini 15–16% na kila njiwa alishwe 50g ya chakula cha nafaka kila siku. Weka chakula mbele ya banda, na kwa ukuaji wa haraka wa vifaranga, wape chakula kwenye maganda ya konokono, chokaa, mifupa iliyosagwa, chumvi, mchanganyiko wa majani, mchanganyiko wa madini na malisho ya kawaida kama vile mboga za majani pamoja na maji safi.

Watoto wa njiwa hupata chakula kutoka kwa mama kwa siku 10, na kisha huanza kuruka ili kujilisha wenyewe. Weka chakula na maji safi karibu na banda, na njiwa huanza kutaga kwa miezi 5–6, hutaga mayai mawili kwa mwezi na kuanguliwa kwa siku 17–18. Magonjwa ambayo huathiri njiwa ni pamoja na mafua, kipindupindu, homa ya tumbo, kideri, mafua na magonjwa yanayosababishwa na upungufu wa lishe.

Mwishowe kwa matokeo bora, fuata ushauri wa daktari wa mifugo, tenganisha ndege wagonjwa na ndege wenyewe afya, chanja kwa wakati, safisha banda na uua viini, wape chakula bora na tumia dawa kuondoa chawa kutoka kwa miili yao.